EMANYATA SECONDARY SCHOOL
P. O. BOX 13 LOLIONDO
ARUSHA- TANZANIA
Website: http://emanyataschool.weebly.com/
Email: emanyattasecondary@gmail.com

**Mzazi/mlezi wa: ……………………………………………**

**YAH:-MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA EMANYATA SEKONDARI KIDATO CHA KWANZA NA VIDATO VINGINE (KWA WANAOHAMIA) MWAKA 2021.**

1. **UTANGULIZI:**

Ninayo furaha kubwa kukukaribisha katika shule ya Sekondari EMANYATA kwa mwaka 2021.

- Hongera sana. Shule hii ambayo ni ya bweni na mchanganyiko, itafunguliwa kwa kidato cha kwanza tarehe **11 Januari, 2021**siku ya Juma tatu.Ili uweze kupokelewa shuleni ni lazima ukamilishe mahitaji yalioorodheshwa katika fomu hii ya kujiunga. Endapo mwanafunzi atakayekuwa amechaguliwa kujiunga na shule yetu na kushindwa kuripoti ndani ya wiki mbili baada ya shule kufunguliwa ama tarehe iliotajwa katika fomu hii basi nafasi yake itatolewa kwa mwanafunzi mwingine wa akiba.

2. **MASOMO**:

Umechaguliwa kuchukua masomo yafuatayo:-English language,Kiswahili,History,Civics, Geography, Biology, Chemistry, Physics, Basic mathematics na Agricultural science.Shule ina vitabu ila havitoshi kwa kila mwanafunzi kuwa na chake kwa kila somo hivyo tunashauri yeyote mwenye uwezo wa kujinunulia vitabu afanye hivyo.Masomo yataanza rasmi mara tu baada ya kufungua shule.

3. **MAHALI SHULE ILIPO**:

Emanyata sekondari ni shule ya jamii ya wafugaji wakazi wa Wilaya ya Ngorongoro.Shule hii inamilikiwa na chombo cha udhamini wa malaigwanani kiitwacho AIGWANAK TRUST na kusimamiwa na shirika la “Pastoral Women Council” (PWC).Shule hii ipo katika kijiji cha Ololosokwan, Kata ya Ololosokwan, Tarafa ya Loliondo, Wilaya ya Ngorongoro.Ipo umbali wa karibia kilomita 52 toka Mji wa Wasso-makao makuu ya wilaya ya Ngorongoro.Emanyata sekondari ni shule ya mchanganyiko (wasichana na Wavulana) na ni ya mchepuo wa sayansi kilimo.Inatoa msisitizo wa wanafunzi wake kuongea lugha ya kiingereza na inatilia mkazo ufundishaji wa masomo ya sayansi kwa vitendo.Pia ina walimu waliobobea na wenye vipaji maalum.Tuna mandhari ya kuvutia na kujifunzia

3.0 **VIFAA VYA KUJA NAVYO SHULENI**

i. Baadhi ya vifaa vya darasani unavyotakiwa kuja navyo
- **Daftari 15** (Counter book Quire 3) na **kalamu** za kutosha
- Madaftari madogo 6 kwa ajili ya mazoezi
- Rula 1
- Mathematical set 1
- Dictionary Oxford – English to English
- **Vitabu binafsi** vya rejea vya masomo yanayofundishwa Sekondari vya kidato husika.
- **Begi** la kubebea madaftari na vitabu (Mifukoya plasitic ni marufuku kuonekana nayo hapa Shuleni)
- **File** kwa matumizi binafsi kwa ajili ya kutunza kumbukumbu za masomo hasa mitihani (Past paper)
- Unatakiwa kuja na**Rim paper** (Karatasi nyeupe) kwa matumizi binafsi hasa kipindi cha majaribio ya wiki na mwezi.

**ii. Vifaa na mahitaji mengine ya Mwanafunzi**
- Vyombo vya kulia chakula (Sahani,Kikombe,Bakuli na kijiko –Sahani za bati (Aluminium) au mifupa
- Taulo ya kuogea/ Kanga pea mbili kwa wasichana
- Ndala za kuogea
- Shuka mbili au zaidi za rangi ya light blue.
- Toilet paper za kutosha kwa matumizi binafsi
- Uje na sanduku la chuma (trunk) lililo imara na kofuli imara.
- Uje na ndoo ya maji ya lita 10 kwa matumizi binafsi
- **MUHIMU SANA**.Uje na Godoro la sponchi la futi $2\frac{1}{2}$ au $3^1/_2$ kwa 6 lenye foronya na aina ya “**TANFORM**”. Aina nyingine ya magodoro yamebainika kusinyaa mapema sana baada kutumiwa.
- Dawa ya meno,Mswaki,Kiwi,Chandarua,Mafuta ya kujipaka,Sabuni miche 3 au Zaidi

iii. Vifaa vya usafi
- Mvulana aje na Jembe lenye mpini na hard broom ngumu kwa ajili ya usafi ya maeneo yao ya usafi watakayopangiwa

Msichana aje na Jembe lenye mpini na Fagio za chelea kwa ajili usafi wa maeneo ya usafi atakayopangiwa

## 4. MAHITAJI MUHIMU YA SHULE NA UTARATIBU WA MALIPO:

i) **Gharama ya fomu**: Unatakiwa kulipa Tsh. 5000/=, ikiwa ni gharama ya fomu ya kujiunga na usajili shuleni(Registration fee).Kiasi hiki kitalipwa wakati wa kuchukua fomu.

ii) **Ada/karo**: Jumla ya karo ya shule kwa mwaka wa masomo ni Tsh. 1,200,000/=.Malipo haya yatalipwa kwa mihula miwili ama mara moja kutegemea uwezo wa mlipaji.Muhula wa kwanza ni Tsh. 600,000/=na wa pili ni Tsh. 600,000/=.ya hani kwa nusu muhula utalipa TSH 300,000 jumla kwa muhula ni 600,000.

**iii)** **Karo ya shule**na **michango yote ya shule** zilipwe Kupitia akaunti ya shule ya sekondari Emanyata benki ya NMB,Tawi la Loliondo.Akaunti nambari: **41102300010** na kuleta **“pay-in-slip”** kwa Mhasibu wa shule tayari kukatiwa stakabadhi.**Hakuna pesa yoyote itakayopolekewa mikononi hata kama ni 5000.**

**MAJUMUISHO YA MALIPO YA KARO YA SHULE NA MICHANGO MENGINE YA SHULE NI KAMA IFUATAVYO.**

| **MALIPO** | | |
|---|---|---|
| **AINA YA MALIPO** | **MUHULA WA I** | **MUHULA WA II** |
| i) KARO | 600,000 | 600,000 |
| ii) MATIBABU(MEDICAL) FEE | 10,000 | 10,000 |
| iii) MCHANGO WA MAABARA | 50,000 | |
| iv) MITIHANI YA NDANI | 10,000 | 10,0000 |
| JUMLA YA ADA NA MICHANGO KWA MWAKA NI **1,290,000/=** | | |

**MUHIMU**:Michango hii haijumuishi ada za Mitihani ya Taifa inayotungwa na Baraza la Mitihani La Tanzania.

**MAHITAJI MENGINE MUHIMU:**

1)SARE ZA SHULE;

a)**msichana;** sketi 2**nyekundu**; suruali 2**nyekundu** ya kuvaa na sketi; sweta**kijani**; ;T-shirt 2 zenye nembo ya shule (zitapatikana shuleni kwa gharama ya Tsh 24,000/= zote mbili), **mvulana**;suruali 2**nyeusi**; sweta 1**kijani**;; T-shirt 2 zenye nembo ya shule (**zitapatikana shuleni kwa gharama ya Tsh 24,000/= zote mbili**) Nguo za kazi(**Shamba dress**) ; wasichana sketi 2 za kaki; wavulana suruali 2 za kaki nguo hizi watavaa na T-shirt hizo zenye nembo ya shule;;Mwanafunzi avae sare wakati akisafiri na anapokuwa shuleni;

**Muhimu**: kwa wanafunzi wanaohamia shule wanapaswa kufanya mawasilianona uongonzi wa shule ili wapewe maelekezo ya **SARE** za madarasa wanaohamia.

**b**) Mwanafunzi aje na shati 2 nyeupe mikono mifupi;

**c)Truck suit** ya Light blue yenye mistari meupe pembeni(inapatikana shuleni kwa garama ya 32,000/= **yenye nembo ya shule.hatupokei truck suit wala t-shirt isiyokuwa na nembo ya shule**, hivyo mwanafunzi aje na fedha shuleni atazikuta.

**d)**Vi**atu vyeusi vya ngozi, vya kufunga na kamba; visigino visiwe** virefu zaidi ya inchi moja na nusu ama vya ghorofa.Viatu visiwe na urembo wa aina yoyote,**Soksinyeupe** jozi mbili kwa wasichana na **nyeusi** kwa wavulana.

**e)**Raba kwa ajili ya michezo;

f) **Ajena Bukta ya michezo**

**f)**Chandarua kwa ajili ya kujikinga na mbu;

**g)**Malapa ya kuogea na ndoo ya kuogea(chipsi);

**h**) Shuka mbili za rangi ya bluu kwa wavulana na nyekundu iliopauka(pink) kwa wasichana;na blanketi moja.

**i)**Vifaa vya usafi; dekio(mopper) moja na squeezer moja;

**j).**Jembe lenye mpini pamoja na fyekeo moja.
**k)**. Daftari kubwa yaani counter books kumi(10),penseli,rula; kalamu za kutosha(za wino bluu ama nyeusi); na bofa aina ya oxford;
**l**). Sanduku imara la bati au chuma na kufuli yake;
M) Aje na godoro lenye ukubwa wa futi 2 na Nusu;
N) Aje na**OXFORD** Dictionary English to English
O. Aje ndoo ndogo ya maji kwaajili kuogea.
P. Mwanafunzi aje na rimu mbili za mwaka mzima kwa ajili ya mazoezi ya kila siku; za **A4-Papers.**

**ANGALIZO:**

- **a)** Mwanafunzi hataruhusiwa kuvaa nguo za nyumbani tofauti na zile zilizoorodheshwa kwenye fomu hii ya maagizo;
- **b)** Mwanafunzi ni lazimza awe na nywele fupi; na haruhusiwi kunyoa kimitindo au kusuka;
- **c)** Kila mzazi au mlezi anatakiwa kufika hapa shuleni na mtoto wake ili amkabidhi kwa uongozi wa shule.Uhakikishe kuwa mwanao hajabeba vyakula;redio;simu au kifaa chochote kinachoathiri masomo au silaha ya aina yoyote ile;Mwanafunzi atakayekuja mwenyewe bila mzazi au mlezi hatapokelewa;
- **d)** Mawasiliano yoyote yanayohusu hali ya mtoto yafanyike kati ya mzazi au mlezi na ofisi ya Mkuu wa Shule;
- **e)** Mwanafunzi atakabidhiwa nakala ya sheria, kanuni na taratibu za shule mara atakapofika shuleni na atapaswa kuzitii na kuzifuata,endapo atazikiuka ataonywa na akiendelea kuvunja sheria za shule atafukuzwa shule.

**SHERIA ZA SHULE: 2021**
Sheria za shule zimetungwa kwa kufuata sheria kuu za nchi na maadili ya kijamii na Kitaifa.Aidha baadhi ya sheria za shule hutungwa kwa kuzingatia mazingira ya shule na kanuni za Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.Hizi zote zinalenga kuboresha uendeshaji wa shule za sekondari kwa ufanisi zaidi.Sheria zote zinalenga kumjenga mwanafunzi kiakili na kimaadili ili hatimaye aweze kulitumikia Taifa kwa uadilifu.

*Mwanafunzi uliyepewa nafasi hii unatakiwa kuzingatia mambo yafuatayo kwa kipindi chote utakapokuwa hapa shuleni;*

- Utii;

- Heshima;
- Usafi wa lugha, mwili na mavazi;
- Kuondoka na urudi shuleni kwa muda ama tarehe zilizopangwa;
- Kufuata kikamilifu ratiba ya shule na kuwahi kukamilisha kazi zote ulizopangiwa;
- Ni wajibu kuhudhuria vipindi vyote tisa kwa siku za masomo;
- Kuwa katika eneo la shule wakati wote na kuomba ruhusa ya kibali cha maandishi ya kutoka nje ya mipaka ya shule kwa siku na muda maalum inapolazimu.Wazazi wanaruhusiwa kuja kuwaona watoto wao Jumapili ya kwanza ya mwanzo wa kila mwezi kuanzia saa 4:00asubuhi hadi saa 10:00 jioni;
- Kulipa ada na michango mingine ya shule kwa wakati ili kukwepa usumbufu usio wa lazima;
- Kufanya majaribio na mitihani yote ya ndani, Timilifu na ile ya Baraza la Mitihani la Tanzania.
- Ni wajibu wa kila mwanafunzi kuwasiliana kwa ama kuzungumza lugha ya kiingereza pindi anapokuwa hapa shuleni.
- Kila mwanafunzi ni lazima avae sare ya shule anapokuwa darasani na anapotoka nje ya shule.Pia awe kwenye shamba dress wakati wote anapokuwa nje ya darasa na siyo vinginevyo.
- Ni wajibu wa kila mwanafunzi kulinda na kutunza mali ya shule.
- Kila mwanafunzi itamlazimu kulala katika bweni alilopangiwa na sio vinginevyo.
- Mwanafunzi haruhusiwi kutembelea nyumba za walimu/watumishi isipokuwa kwa kibali maalumu.
- Ni marufuku kwa mwanafunzi yeyote kuleta vyakula shuleni;
- Mwanafunzi haruhusiwi kuingia ofisi za walimu au ofisi ya mkuu wa shule bila kibali maalum.
- Mwanafunzi haruhusiwi kuingia jikoni na kula chakula kabla ya muda wa kula labda iwe ni kwa kibali maalum.
- Ni marufuku mwanafunzi kuwa na simu ya kiganjani shuleni.
- Mwanafunzi anapokuwa shuleni ni sharti awe ama akae sehemu za wazi na sio mafichoni ama gizani.
- Ni marufuku mwanafunzi kuja shuleni na silaha ya aina yoyote ile.

**MAKOSA YANAYOWEZA KUMFUKUZISHA MWANAFUNZI SHULE NI PAMOJA NA YAFUATAYO:**

- Ulevi,uvutaji sigara, dawa za kulevya, uvutaji bangi n.k.
- Kupigana au kumsababishia mwanafunzi mwingine majeraha;
- Kushawishi au kushiriki katika mgomo wa aina yoyote ile;
- Kubeba au kubebesha mimba;
- Uasherati au kuwa na uhusiano wa kimapenzi ndani na nje ya shule;
- Wizi;
- Kuoa au kuolewa;
- Ubakaji.

**MAKOSA YANAYOMSABABISHA MWANAFUNZI KUSIMAMISHWA MASOMO (SUSPENSION):**

- Kugombana au kutoa maneno machafu;
- Kukataa adhabu;
- Mwanafunzi wa kike kumfulia nguo mwanafunzi wa kiume;
- Kuonesha dharau kwa watumishi au kwa wanafunzi wengine;
- Kutembelea bweni la jinsi nyingine bila kibali maalum;
- Kutembelea vilabu vya pombe, kumbi za starehe, kambi za kitalii bila kibali maalum,nyumba za kulala wageni yaani Guest house n.k.
- Kupika shuleni bila kibali maalum;
- Utoro

**9. MAELEZO MENGINE KUHUSU SHULE YA SEKONDARI EMANYATA:**
***I. Mahali shule ilipo (usafiri):***

Emanyata sekondari ni shule ya jamii ya wafugaji wakazi wa Wilaya ya Ngorongoro.Shule hii inamilikiwa na chombo cha udhamini wa malaigwanani kiitwacho AIGWANAK TRUST na kusimamiwa na shirika la Pastoral Women Council (PWC).Shule hii ipo katika kijiji cha Ololosokwan, Kata ya Ololosokwan, Tarafa ya Loliondo, Wilaya ya Ngorongoro.Ipo umbali wa karibia kilomita 52 toka Mji wa Wasso-makao makuu ya wilaya ya Ngorongoro.Emanyata sekondari ni shule ya mchanganyiko (wasichana na Wavulana) na ni ya mchepuo wa sayansi

kilimo.Inatoa msisitizo wa wanafunzi wake kuongea lugha ya kiingereza na inatilia mkazo ufundishaji wa masomo ya sayansi kwa vitendo.Pia ina walimu waliobobea na wenye vipaji maalum.Tuna mandhari ya kuvutia na kujifunzia.

**II. LIKIZO:**Kila mwanafunzi atapaswa kwenda likizo ama kuondoka shuleni kama itakavyopangwa na shule labda iamuliwe vinginevyo na uongozi wa shule kwa wanafunzi waishio kwenye mazingira hatarishi.Hata hivyo mwanafunzi atatakiwa awe amemaliza kulipa ada ya shule na kurudisha vifaa na vitabu vya shule kabla hajaondoka.Wazazi na walezi mnakumbushwa kuandaa nauli mapema na kushirikiana na uongozi wa shule kuweka utaratibu mzuri na salama wa kuwasafirisha wanafunzi wakati wa likizo ili kuwaepusha kuingia katika mitego vishawishi.
Natumia fursa hii kukukaribisha sana hapa shuleni Emanyata Sekondari na ni
matarajio yangu kuwa ufikapo hapa shuleni utaitumia vyema nafasi hii ya kipekee
kwa kujifunza kwa dhati. Asante sana na karibu Emanyatta.

**………………….**

**SOMOINE JEREMIAH**
**Mkuu wa Shule**

**Mawasiliano : 0692168338/ 0768571209.**

**PRESEDENT OFFICE**

**REGINAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**

**NGORONGORO DISTRICT**

**EMANYATA SECONDARY SCHOOL**

**MEDICAL EXAMINATION FORM 2021**

**To be completed by medical officer only Name of student ………………………………….Age…………………………..**

1. **HIV test………………………………………………………………………………**
2. **Blood count [white & red…………………………………………………………….**
3. **Urine examination……………………………………………………………………..**
4. **UTP…………………………………………………………………………………………..**
5. **Stool examination……………………………………………………………………………**
6. **Syphilis test……………………………………………………………………………………..**
7. **TB test…………………………………………………………………………………………..**
8. **Ear test……………………………………………………………………………………………………**
9. **Eye test…………………………………………………………………………………………………….**
10. **Abdomen………………………………………………………………………………………………**
11. **Spleen……………………………………………………………………………………………………**
12. **Additional information or any other physical ,mental hereditary or infections diseases**

**……………………………………………………………………………………………………………………**

**[Please state nature of treatment]**

**Medical certificate**

**I certify that the above mentioned student has been examined and found him/her to be fit /unfit to pursue further education.[delete whichever not needed**

**Name…………………………………………………..signature……………………….**